## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI MACHI, 2025 NA MWELEKEO KWA MWEZI APRILI, 2025.

### Dondoo za tathmini ya Machi, 2025 na mwelekeo wa Aprili, 2025:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Machi, 2025 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Aprili, 2025 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Machi, 2025 maeneo mengi ya nchi yalipata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo hususan kuanzia wiki ya pili ya mwezi. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo na kusababisha athari ikiwemo mafuriko na kutuama kwa maji.

ii. Katika kipindi cha mwezi Aprili 2025, mvua za msimu zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Kwa upande mwingine, joto linatarajiwa kupungua kiasi katika baadhi ya maeneo.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI, 2025.


Katika kipindi cha mwezi Machi 2025, maeneo mengi nchini yalipata vipindi vya mvua iliyoambatana na ngurumo hususan kuanzia wiki ya pili ya mwezi. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo na kusababisha mafuriko, kutuama kwa maji, uharibifu wa miundombinu na mali na kuathiri shughuli za kiuchumi. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 151.8 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Musoma (mkoa wa Mara) mnamo tarehe 19 Machi, ikifuatiwa na milimita 135.8 katika kituo cha Katema siku hiyohiyo na milimita 129.4 katika kituo cha Mtwara mnamo tarehe 11 Machi, 2025. Vituo vilivyopima mvua milimita 50 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1.

Kwa upande mwingine, upungufu kidogo wa hali ya joto ulijotokeza katika baadhi ya maeneo hususan siku za mvua.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 02/2023*




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 50 au zaidi katika mwezi Machi, 2025

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI APRILI, 2025

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la Bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la chini kidogo ya wastani kwa mwezi Aprili, 2025. Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi, karibu na Pwani ya Afrika mashariki, linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, wakati eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la bahari la juu kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuongeza upepo wenye unyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea ukanda wa pwani pamoja na maeneo jirani. Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuchangia kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi yetu. Migandamizo mikubwa

ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kuimarika kidogo na kupelekea Ukanda mvua (ITCZ) kusogea kuelekea kaskazini.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2025

Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2025 mvua za msimu zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini na kusababisha mafuriko, kutuama kwa maji na kuathiri shughuli za kiuchumi. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kupungua kidogo, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua. Aidha katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kuwa na upungufu wa mvua hali ya joto inatarajiwa kuendelea. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache hususan katika wiki ya kwanza na ya pili.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika maeneo machache katika wiki ya pili ya mwezi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa kati ya wiki ya kwanza na ya pili katika maeneo machache.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza ya mwezi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI MEI, 2025

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2025 vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini, hususan maeno yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

## 2.4 USHAURI

Mvua zinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza, hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 02/2023*

Imetolewa tarehe 01 Aprili, 2025 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz